


**M**bolea sanisi zina athari hasi za muda mrefu kwenye mazingira ambazo ni:

- **zinaua viumbe hai vyenye manufaa kwenye udongo** – viumbe hai hivi ni vidogo sana na hugeza taka kuwa virutubisho - vyenye matamahuluku nyingi, ambazo ni chakula cha mimea;
- **zikitumika kwa wingi zaidi** – huongeza kiasi cha chumvi kwenye udongo na kuunguza mizizi, na kusababisha mimea kukua taratibu, kupoteza maji na hatimaye kufa;
- **zinaongeza kiasi cha naitrate kwenye udongo** – mimea iliyopandwa kwenye udongo huu itakuwa ni sumu kwa binadamu;
- **zinaharibu uwezo wa udongo kuvunjika vunjika** – ni udongo pekee uliovunjika vunjika ambao unaweza kufyonza maji;
- **zinaingia kwenye vijito, mito na maziwa** – ambapo zinaharibu/vuruga mfumo wa mazingira ya maji na kusababisha uchafuzi wake;
- **zinapenya kwenye maji yaliyo aridhini na chini ya ardhi** – bila ya kutoa faida kwa mimea;
- **zinasababisha magonjwa mbalimbali kwa mimea**; na
- **zinatoa matunda na mboga mboga zenye virutubisho vichache na ladha kidogo zaidi.**



dutracelho.com

ATHARI ZA  
MBOLEA SANISI KWA

**MAZINGIRA**